

**OFISI YA JICA
YATIMIZA MIAKA 30
NCHINI TANZANIA
[1980-2010]**



Daraja la Selander ambalo ujenzi wake ulianza mwaka 1980

***Japan International Cooperation Agency
TanzaniaOffice
2010***

JICA Tanzania Office

Ghorofa ya 3, Jengo la Barclays, 1008/1 Mtaa wa Ohio
S.L. P 9450, Dar es Salaam,
Simu: +255-22-2113727-30, Nukushi: +255-22-2112976
Tovuti: <http://www.jica.go.jp/tanzania/english/>

(Picha ya mbele:1982, Kajima)

Yaliyomo

Ujumbe kutoka Serikali ya Tanzania.....	2
Ujumbe kutoka Ofisi ya JICA Tanzania.....	3
1. ODA ya Japani na JICA.....	4-5
2. Miaka 30 ya Ofisi ya JICA Tanzania.....	6-7
3. Shughuli za JICA kwa njia mbalimbali	
(1) Miradi ya Ushirikiano wa kiufundi.....	8-9
(2) Mikopo ya ODA.....	10-11
(3) Misaada isiyokuwa na Masharti ya Kulipa.....	12-13
(4) Mpango wa Mafunzo ya Kiufundi.....	14-15
(5) Wafanyakazi wa kujitolea kutoka Japan.....	16-17
4. Shughuli za JICA Kisekta	
(1) Sekta ya Kilimo.....	18-19
(2)Sekta ya Miundombinu: Usafiri.....	20-21
(3)Sekta ya Miundombinu: Nishati.....	22-23
(4)Sekta ya Miundombinu: Maji.....	24-25
(5)Sekta ya Utawala.....	26-27
(6) Sekta ya Afya.....	28-29
Mipango na Miradi ya JICA Tanzania kwa sasa.....	30

Ujumbe kutoka kwa Bw. Ramadhani M. KHIJJAH
Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Uchumi
Kuadhimisha Miaka 30 ya Ofisi ya JICA Tanzania



Kwa furaha kubwa, ninaipongeza JICA kwa kutimiza miaka 30 ya Ushirikiano wa Maendeleo baina yake na Tanzania.

Ninapenda kuchukua fursa hii, kwa niaba ya Serikali na watu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kutoa shukrani zetu kwa Serikali ya Japani kupitia JICA, kwa kuunga mkono jitihada zetu za kitaifa za kuleta maendeleo.

JICA kwa kiasi kikubwa imechangia katika juhudzi za Serikali ya Tanzania za kukuza uchumi na kupunguza umasikini. Misaada ya JICA nchini unajumuisha; misaada bila masharti, misaada ya kiufundi, kufadhili miradi kwenye maeneo ya vipaumbele kwa serikali hususan katika sekta za kilimo, miundombinu ya barabara, maji, nishati, utawala na afya.

Mathalani, katika kutambua umuhimu wa Sekta ya Kilimo nchini Tanzania, JICA imekuwa ikiisaidia Serikali kuanzisha miradi ya umwagiliaji maji na kutoa msaada wa kiufundi ili kuongeza uzalishaji kwenye sekta hiyo. Vivyo hivyo, JICA imekuwa ikisaidia uboreshaji na ukarabati wa barabara jijini Dar es Salaam; pia ujenzi wa barabara kuu katika miji mikubwa nchini. Msaada wa JICA usiopimika katika kuboresha barabara zetu, umechangia kwa kiasi kikubwa kukuza shughuli za kiuchumi kwa kuwezesha usafirishaji wa watu na bidhaa kwa urahisi na usalama.

Tanzania inathamini mahusiano haya bora na ya miaka mingi baina yake na Japani na JICA. Tunatazamia mahusiano imara zaidi kwa miaka ijayo, tunapoainisha vipaumbele vyetu katika maendeleo, ambavyo vitawezesha Japani hususan JICA, kupata upenyio na kutumia utaalami wao ulio dhahiri, kuleta msukumo katika juhudzi zetu za kijamii na kiuchumi.

Kwa kumalizia ujumbe wangu, napenda kurudia kuipongeza JICA kwa kutimiza miaka 30, pia tunatoa shukrani zetu za dhati kwa wafanyakazi wa JICA kwa moyo wao wa kujitoa katika kuchangia ajenda yetu ya kitaifa ya kukuza na kuboresha hali ya maisha ya watu wetu.

Ujumbe Kutoka kwa Bw. Yukihide KATSUTA

Mwakilishi Mkuu wa JICA nchini Tanzania

Tunapoadhimisha miaka 30 tangu kufunguliwa kwa ofisi ya JICA nchini Tanzania, ningependa kuchukua nafasi hii kuwashukuru Watanzania wote na Serikali kwa msaada mkubwa waliotupatia katika shughuli zetu hapa nchini.



Inafahamika kwamba ufunguzi rasmi wa ofisi za JICA nchini Tanzania mnamo mwaka 1980, ni tukio muhimu katika historia ya urafiki kati ya Japani na Tanzania. Hata hivyo, ufunguzi huu haukuwa mwanzo wa mahusiano ya Japani na Tanzania, bali ulikuwa ni mwendelezo wa historia ndefu ya ushirikiano ulioanza mwaka 1962 pale Mtanzania wa kwanza alipokubaliwa kushiriki mafunzo nchini Japani. Tangu hapo shughuli za JICA nchini zimeendelea kukua na kupanuka mwaka hata mwaka, kuanzia ushirikiano wa kiufundi hadi msaada wa fedha bila masharti na mikopo.

Falsafa ya JICA kutoa ushirikiano nchini imejikita katika kuunga mkono jitihada za Watanzania katika kujiletea maendeleo yao wenyewe kwenye sekta za kijamii na kiuchumi. Kwa muktadha huo, misaada ya JICA kwa Tanzania inaenda sanjari na Dira za Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2025 na 2020 na pia Mikakati ya Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania, MKUKUTA na MKUZA. Katika kipindi chote hiki cha ushirikiano, JICA imekua inatoa ushirikiano wake katika misingi ya kuaminiana na kuheshimu matakwa wa Serikali ya Tanzania na watu wake. JICA itaendelea kufanya hivyo katika siku zizajoz.

Ninaamini kwamba kitini hiki kitakuza uelewa wako wa kazi za JICA nchini Tanzania. Aidha ni matarajio yetu kwamba utaendelea kutupatia msaada na ushirikiano stahiki katika shughuli zetu ambazo kwa hakika zinalenga kuboresha hali ya maisha ya watu wa Tanzania.

Udumu Urafiki kati ya Japani na Tanzania.


1. ODA ya Japani na JICA

JICA ni Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japani ambalo linalosimamia misaada inayotolewa na Serikali ya Japani (ODA) kwa nchi zinazoendelea.

Tangu kuanzishwa kwake mnamo mwaka 1974, Shirika hili limekuwa likitoa misaada ya aina mbalimbali katika nchi na maeneo mbalimbali zaidi ya 150. Majukumu ya JICA yamekuwa yakibadilika kutokana na wakati.

Sanjari na dira yake ya “Maendeleo ya Kasi na kwa Wote” (Inclusive and Dynamic Development), JICA imekuwa ikishughulikia masuala ya nchi zinazoendelea kwa kutumia njia muafaka za misaada na kwa kuzingatia tatizo, eneo na nchi husika.

Majukumu ya JICA yamekuwa ya kiutendaji zaidi na kwa hiyo imekuwa ikifanya kazi karibu zaidi na nchi washirika, wafadhili wa kimataifa, na mashirika binafsi. Zaidi ya yote JICA imekuwa ikishirikiana na wananchi pamoja na jamii, huku ikiwapa tumaini la siku za usoni.



Misaada ya Japan kwa Tanzania <miaka 5 iliyopita> million JPY (Yen=15Tsh)

	2004	2005	2006	2007	2008
Ushirikiano wa Kiufundi	2,287	2,411	2,444	2,136	2,009
Misaada bila Masharti	-	-	8,857	2,000	2,000
Mikopo ya ODA	2,372	1,837	3,776	5,705	6,304
Jumla kwa mwaka	4,659	4,248	15,077	9,841	10,313

DIRA

Maendeleo ya Kasi na kwa Wote

Dhima

- Kushughulikia mada za kimataifa
- Kupunguza umasikini kwa kukuza uchumi
- Kuboresha Utawala Bora
- Kuleta uhakika wa maisha (human security)

Mkakati

- Msaada unaojumuisha kila mtu
- Msaada usiokuwa na Masharti
- Kuhamasisha ushirikiano katika maendeleo
- Kuendeleza tafiti na kushirikishana utaalamu



Mradi wa Maji Lindi

2. Miaka 30 ya Ofisi ya JICA Tanzania [1980-2010]

Ingawaje ofisi ya JICA ilifunguliwa nchini Tanzania mwaka 1980, ushirikiano kati ya Japani na Tanzania ulianza mwaka 1962 pale Watanzania ulipoanza kushiriki mafunzo nchini Japani, na vilevile Japani kuleta wataalamu wake nchini Tanzania mwaka 1965.

Aidha mwaka 1966, mpango wa wafanyakazi wa kujitolea kutoka Japani (JOCV) ulianzishwa na mwaka huo huo, ofisi ya idara hiyo ilifunguliwa jijini Dar es Salam. Kwa kadri mahusiano kati ya Japani na Tanzania yalivyozidi kupanuka, JICA iliipandisha hadhi ofisi ya JOCV na kuwa ofisi kamilii ya JICA mwaka 1980.



Daraja la Selander - Mradi wa kwanza wa barabara kufadhiliwa na Japani jijini Dar es Salaam, na ujenzi wake ulianza mwaka 1980 (Mchoro wa kubuni kazi)



(picha:1996,
Inage/JICA)



(picha:1997, Ofuchi/JICA)

Mkakati na Mpango wa sasa wa JICA nchini Tanzania

Malengo ya Japani/JICA nchini Tanzania ni kujenga na kuhamsisha ukuzaji wa uchumi na upunguzaji wa umaskini kwa kusaidia utekelezaji wa MKUKUTA/MKUZA.

Nguzo za ushirikiano ni (a) kuendeleza na kukuza uzalishaji bora kwa kusaidia maendeleo ya miundombinu na kilimo, (b) kuendeleza utawala bora kwa kujengea uwezo mifumo ya utawala na usimamizi wa fedha. Aidha JICA inaendelea kusaidia sekta za afya na elimu.

Katika kukabiliana na changamoto zinazoikumba Tanzania, JICA inatumia njia mbalimbali kama vile misaada, mikopo, ushirikiano wa kiufundi ikiwa ni pamoja na uletaji wa wafanyakazi wa kujitolea. Vile vile JICA inaimarisha ushirikiano wake ili ushabihiane na wafadhili wengine wa maendeleo pamoja na Serikali ya Tanzania sanjari na uratibu wa misaada (aid coordination).

3. Shughuli za JICA kwa njia mbalimbali:

(1)Miradi ya Ushirikiano wa Kiufundi

Ushirikiano wa kiufundi ni moja ya miradi mikuu katika shughuli za JICA ulimwenguni.

Ushirikiano huu umekuwa unahusu uletaji wa wataalam, utoaji wa mafunzo nchini Japani na kwingineko na utoaji wa vifaa na mitambo kwa lengo la kuboresha utendaji na taratibu za kiutawala katika nchi zinazoendela.

Mtaalamu wa kwanza wa kijapani alikuja nchini Tanzania mnamo mwaka 1965 katika nyanja ya mazao yatokanayo na mianzi (bamboo products). Kupitia ushirikiano wa kiufundi katika nyanja za kilimo, afya, maendeleo ya miundo mbinu na nyinginezaji, JICA inasaidia kukuza uwezo wa Watanzania kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na uchumi wa Tanzania.



Mtaalamu wa kijapani akiwa katika kituo cha maendeleo ya vi-wanda mkoani Kilimanjaro (picha:1986, Fujii/JICA)



Mtaalamu wa kijapani akiwa na wanakijiji wa Pongwe mkoani Tanga, kwenye Mradi wa afya ya mama na mtoto (picha:1999)



Skimu ya umwagiliaji maji katika Taasisi ya Mafunzo ya Wizara ya Kilimo Ilionga iliboreshwaa kama maandalizi ya mafunzo ya kilimo cha mpunga, kupitia mradi wa Ushirikiano wa Kiufundi wa JICA (picha:2009)

(2) Mikopo ya ODA

Kwa kutumia ODA, Japani inasaidia nchi zinazoendelea kwa kutoa mikopo yenye riba kidogo na ya muda mrefu kwa ajili ya kugharimia jitihada zao za maendeleo. Mpango huu unawezesha utumiaji bora wa fedha zilizokopwa na usimamizi sahihi wa miradi inayofadhiliwa na hivyo kuhakikisha nchi zinazoendelea zinamiliki mchakato wa maendeleo yao.

Nchini Tanzania, mikopo ya namna hii imekuwa ikitolewa kwa miradi mikubwa ya maendeleo ya miundombinu, kama vile umwagiliaji, upatikanaji wa nguvu za umeme, mawasiliano, n.k tangu mwaka 1978. Kwa sasa, mradi wa maendeleo ya barabara kuu inayounganisha Tanzania na Kenya uko kwenye utekelezaji chini ya mpango huu.



Mradi wa ujenzi wa barabara ya Arusha-Namanga-Mto Athi ambayo inaendelea kujengwa kupitia misaada ya ODA kutoka Japani unatarajiwa kukamilika mwaka 2011 (picha:2009)



Skimu ya umwagiliaji maji Moshi vijijini, uliojengwa kwa mikopo ya ODA toka Japani miaka ya 80. Katika eneo hili, tangu miaka ya 1970 wataalamu wa kijapani wametoa misaada ya kiufundi kwa Chuo cha Mafunzo ya Kilimo Kilimanjaro ambacho kilijengwa na Japani kupitia misaada bila masharti (Grant Aid)

Misaada ya Mikopo ya Kibajeti (General Budget Support)

Kupitia misaada hii, JICA pamoja na wafadhili wengine 14 wa maendeleo, wamekuwa wakitoa fedha kusaidia bajeti ya serikali ya Tanzania. Mpango huu ni utaratibu mzuri ambao hutoa nafasi ya ku-changia bajeti ya serikali na hivyo kuiwezesha serikali kutekeleza mikakati yake ya kukuza uchumi na kupunguza Umasikini (MKUKUTA / MKUZA)

(3) Misaada isiyokuwa na Masharti ya Kulipa

Hii ni misaada ya utoaji fedha kwa nchi zinazoendelea bila sharti la kulipa. Lengo ni kushiriki katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii, kwa kusaidia nchi inayopokea msaada kuanzisha na kuboresha huduma na vitendea kazi.

Nchini Tanzania miradi mingi hasa ya miundombinu, kama vile barabara, umeme, maji pamoja na kilimo, afya na elimu imetekelezwa kuititia aina hii ya misaada.

Maboresho mengi ya barabara kuu jijini Dar es Salaam yamefanyika kuititia misaada ya aina hii kutoka Japani.



*Soko la samaki Magogoni Dar es Salaam lilijengwa 2000
(picha:2004, Funao/JICA)*



Madaraja manne katika barabara kuu kati ya Mtwara na Lindi yaliyengwa kwa msaada kutoka Japani kufuatia uharibifu mkubwa uliosababishwa na mafuriko mwaka 1990. Mradi huu umerahisisha usafiri katika eneo hili (picha:2010)



Madarasa yaliyojengwa katika Shule za Msingi jijini Dar es Salaam (picha:2001, Konoike)

(4) Mpango wa Mafunzo ya Kiufundi

Mpango wa mafunzo unahusisha utoaji wa ujuzi/teknolojia kupitia mafunzo kwa maafisa tawala, mafundi sanifu na watafiti. Huu ni mpango mkuu wa maendeleo ya rasilimali watu unaoteklezwa na JICA.

Mtanzania wa kwanza alishiriki kwenye mafunzo Japani mwaka 1962. Kuanzia wakati huo, takribani Watanzania 8,000 wamehudhuria mafunzo nchini Japani, Tanzania na katika nchi nyingine kama Malaysia, Singapore, Misri n.k na hivyo kuweza kubadilishana uzoefu/ujuzi kutoka kwa watu wa nchi nyingine zinazoendelea.

Baada ya mafunzo haya, washiriki hujiunga na Chama cha Watanzania waliopata mafunzo nchini Japani chini ya JICA (JATA) na huendelea kushirikishana uzoefu na washiriki waliopita na hivyo kuchangia maendeleo ya jamii.



Walimu wa Sayansi na Hesabu kutoka nchi mbalimbali za Asia na Afrika wakiwa katika mafunzo huko Malaysia (picha:2008)



Mshiriki Mtanzania katika kozi ya Utawala kwa ajili ya Maendeleo na Mipango ya Mikoa, Bw. Ado Mapunda, akiwa kwenye maonyesho ya utamaduni nichini Japani (picha:2005)



Wauguzi ambao ni mionganoni mwa wanachama wa JATA wakibadilishana uzoefu katika warsha juu ya PMTCT (picha:2010)

(5) Wafanyakazi wa Kujitolea kutoka Japan

Mpango wa kuleta wafanyakazi wa kujitolea wa JICA, yaani JOCV, ulianzishwa kwa madhumuni ya kutumia ujuzi wa kiufundi na uzoefu wenye tija wa wafanyakazi hao kwa manufaa ya watu wa nchi zinazoendelea.

Kundi la kwanza la wafanyakazi hawa liliwasili nchini Mwaka 1967. Kundi hili lilijumuisha wataalamu 24 wa ushonaji na 6 wakiwa na utaalamu wa bustani. Wafanyakazi wa kujitolea (JOCVs) wanaweza kuletwa kwa kikundi kwa kufanya kazi katika miradi mbalimbali. Kati ya mwaka 1986-1998, JOCVs 40 walifanya kazi katika mradi mmoja mjini Dodoma uliojulikana kama "Green Cooperation Project", na kati ya mwaka 1992-97, wafanyakazi wengine 17 waliperekwa kufanya kazi katika Ilonga, mkoa wa Morogoro, kama wauguzi, wataalamu wa lishe na maafisa maendeleo vijijini.

Tangu kuanzishwa kwa mpango huu, takribani JOCVs 1300 wame-shaletwa nchini kufanya kazi katika maeneo na nyanja mbalimbali kama vile: kilimo na uvuvi, elimu, afya, umakenika na kazi za kijamii.



Mmoja katika kundi la kwanza la JOCV akimfundisha mwana-funzi mbinu za ushonaji (picha:1967)



*Mfanya kazi wa
kujitolea akisaidia
matengenezo ya simu
jijini Dar es Salaam
(picha:1994,
Watanabe/JICA)*



*Muuguzi ambaye ni mmoja wa wafanyakazi wa kujitolea kutoka
Japoni akimhudumia mgonjwa Ilonga (picha:1997, Watanabe/JICA)*

4. Shughuli za JICA Kisekta:

(1) Sekta ya Kilimo

Japani inatambua kilimo kama moja ya eneo la kipaumbele katika ushirikiano wake na Tanzania.

Ushirikiano wa JICA katika sekta hii ulianza miaka ya sabini baada ya Japani kuleta wataalamu wa kilimo nchini. Miaka ya themanini, Japani iliweka mkazo katika kilimo cha mpunga hususan katika maeneo ya Kilimanjaro, kwa kusaidia ujenzi wa kituo cha kilimo kuititia misaada bila masharti na skimu ya umwagiliaji maji kuititia mkopo wa ODA. Japan pia imekuwa ikitoa msaada wa kitaalam tangu miaka ya themanini na hivyo kufanikisha ongezeko kubwa la uzalishaji wa mpunga katika mashamba ya mifano.

Moja ya miradi inayoendelea una lengo la kueneza mafanikio haya katika maeneo mengine mengi nchini kwa kuimarisha mfumo wa uenezaji ufundi wa kilimo cha umwagiliaji maji.



*Wakulima wakivuna mpunga katika skimu ya umwagiliaji maji
Moshi vijijini (picha:2007)*



Mtaalam wa kijapani akielekeza wakulima jinsi ya kulima mpunga kwa kutumia trekta katika skimu ya umwagiliaji maji Moshi vijijini (picha:1986, Fujii/JICA)



Mafunzo “kutoka kwa mkulima kwenda mkulima mwingine”: Mafunzo ya JICA yanazingatia masuala ya jinsia na uboreshaji endelevu wa maisha ya mkulima (picha:2005)

(2) Sekta ya Miundombinu: Usafiri


Sekta ya miundombinu ikijumuisha barabara, ni eneo jingine la kipaumbele katika ushirikiano wa JICA na Tanzania.

JICA imekuwa ikisaidia sekta hii tangu miaka ya sabini kwa kuboresha na kukarabati barabara kupitia miradi mbalimbali ya misaada bila masharti na mikopo ya ODA. Misaada hii imeelekezwa katika maeneo ya mijini kama Dar es Salaam na katika ujenzi wa barabara za kuunganisha miji mikubwa. Hii imerahisisha usafirishaji wa mizigo na watu katika maeneo hayo.

Vilevile JICA inatoa ushirikiano wa kiufundi katika sekta hii.



Mtaalam wa kijapani katika mpango kabambe wa maendeleo akiwasilisha mada kwa wadau. JICA iliisaidia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kutafiti na kuandaa mpango kabambe wa usafiri katika jiji hilo (picha:2008)



Misaada kutoka Japani kwa ajili ya uboreshaji wa usafiri jijini
Dar es Salaam (mchoro na JICA Tanzania)

(3) Sekta ya Miundombinu: Nishati

Kwa zaidi ya miongo mitatu sasa, JICA imekuwa moja ya washirika wakuu wa maendeleo katika sekta ya nishati nchini Tanzania; kazi zake zote zimekuwa zikitekelezwa kwa ushirikiano na TANESCO.

JICA imekuwa ikiweka mkazo katika mpango mpya na bora wa ugavi na usambazaji umeme katika mikoa ya Dar es Salaam na Kilimanjaro, na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya viwanda vikuu na kurahisisha upatikanaji wa umeme kwa wananchi.

Kwa jitihada hizi hali ya upatikanaji wa umeme imekuwa bora zaidi ikilinganishwa na miaka 30 iliyopita.



Wahandisi wa kijapani wakiwa na wahandisi wa TANESCO katika mradi wa kuhuisha na kurekebisha mfumo wa usambazaji wa umeme Dar es Salaam (picha:1986, Fujii/JICA)



Moja ya vituo vidogo vya umeme katika eneo la Kilimanjaro vilivyojengwa mwaka 1985 chini ya mradi wa ugavi na usambazaji umeme mkoani Kilimanjaro (picha:2009)



Vifaa vya ugavi na usambazaji wa umeme Dar es Salaam (picha:1999)

(4) Sekta ya Miundombinu: Maji

Katika kuboresha upatikanaji wa maji safi na salama maeneo ya vijiini, JICA imetua misaada katika kutengeneza mipango ya maendeleo kwenye vyanzo vya maji na katika usambazaji wa maji. Aidha JICA imetua misaada katika kuchimba visima katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Dar es Salaam, Pwani, Mara na kwingineko.

Zaidi ya hayo, JICA inasaidia kukuza uwezo wa Halmashauri za Serikali za Mitaa katika kutoa huduma ya maji safi na maji taka, na vilevile katika kuboresha uwezo wa ofisi za maji katika usimamizi wa vyanzo vya maji.

Mjini Zanzibar, JICA inatoa misaada ya kuboresha miundombinu ya maji na kuanzisha utaratibu wa ukusanyaji wa ankara za maji mjini.



Wanakijiji wakiangalia kwa shauku kubwa ya maji kazi ya uchimbaji kisima Mtwara (picha:2005)



Mfanyakazi wa mradi wa maji akiwafundisha viongozi wa kijiji uendeshaji na usimamizi wa fedha kwa lengo la kutunza miundombinu ya maji (picha:2006)



Katika mkoa wa Kagera, huduma za maji katika maeneo yaliyoathiriwa na wakimbizi ziliboreshwa kwa kupitia misaada ya Japani mwaka 1996 (picha:2008)

(5) Sekta ya Utawala

Kwa miongo kadhaa sasa, JICA imekuwa ikiunga mkono jitihada za serikali ya Tanzania katika kuboresha utoaji wa huduma na uwajibikaji kwa umma kupitia mpango wa mafunzo nchini Japani. Zaidi ya watumishi wa umma 500 wamepata mafunzo katika nyanja za utumishi wa umma, usimamizi wa fedha, teknolojia ya habari, takwimu, utawala wa polisi n.k.

Hivi karibuni, JICA imepanua msaada wake wa fedha kusaidia Mpango unaoendelea wa Marekebisho ya Usimamizi wa Fedha za Umma na Mpango wa Marekebisho ya Serikali za Mitaa.

Vilevile JICA inasaidia uboreshaji wa shughuli za ukaguzi wa mahesabu ya ndani, maboresho ya usimamizi wa mpango wa mafunzo kwa Serikali za Mitaa, mchakato shirikishi katika ngazi za chini kupitia ushirikiano wa kiufundi.



JICA ilianzisha mafunzo ya maboresho ya Serikali za Mitaa huko Osaka kuanzia mwaka 2002– 2006 yakihuisha Ofisi ya Waziri Mkuu — TAMISEMI na viongozi wa Serikali za Mitaa kutoka Tanzania. Kuanzia mwaka 2007, JICA imepanua mafunzo haya na kujumuisha Kenya, Uganda na Zambia. (picha:2008)



Mkutano wa kwanza wa Chama cha Tanzania na Osaka ambacho kilianzishwa mwaka 2006 kwa lengo la kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali za Mitaa na hivyo kueneza yale mazuri waliyofunza Japani (picha:2008)



Mafunzo ya wahamasishaji wa mchakato wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O and OD) ambayo yalifanyika kupitia ushirikiano wa kiufundi wa JICA (picha:2010)

(6) Sekta ya Afya

Tangu miaka ya sabini Japani imekuwa ikiisaidia Serikali ya Tanzania katika sekta ya afya kwenye maeneo mbalimbali kama vile Afya ya Mama na Mtoto, VVU/UKIMWI, Malaria na katika kuboresha sekta ya afya.

Aidha JICA imekuwa ikitoa ushirikiano wa kiufundi katika kitengo cha watoto cha Hospitali ya Taifa Muhimbili ili kuboresha matibabu kwa watoto (Lab-Based Medicine and Acute Paediatric) tangu mwaka 1994, kwa kuleta madaktari.

Vile vile madaktari wa watoto na wauguzi kote nchini wamekuwa wakipatiwa mafunzo ndani ya Tanzania kwa msaada wa JICA ili kuboresha elimu na ujuzi wao.



*Wauguzi wakiwa katika warsha ya matibabu kwa watoto
(picha:2005)*



Mtaalamu wa JICA katika kitengo cha afya ya mama na mtoto
katika hospitali ya Muhimbili (picha:1997, Ofuchi/JICA)

Kabla



5S

Baadaye



JICA inasaidia kuboresha mazingira ya kazi kwa kutumia kanuni ya
“5S (Sasambua, Seti, Safisha, Sanifisha, Shikilia)” kama msingi wa
kuboresha huduma za afya katika hospitali kadhaa nchini

Current JICA's Programmes and Projects in Tanzania

< January 2011>

T: Technical Cooperation, G: Grant Aid, L: ODA Loan

Programme / Project	Type	Area	Period
(1) Agriculture			
Strengthening the Backstopping Capacities for the DADP Planning and Implementation	T	Whole Country	2009.3-2012.3
ASDP Basket Fund	G	Whole Country	2006.7-2010.6
Capacity Development for the ASDP Monitoring and Evaluation Systems	T	Dar, Morogoro, Dodoma	2008.3-2011.3
Supporting Delivery Systems of Irrigated Agriculture (TANRICE)	T	Whole Country	2007.6-2012.6
Capacity Development for the Promotion of Irrigation Scheme Development under DADPs	T	Whole Country	2010.12-2013.11
(2) Infrastructure (transportation)			
Capacity Strengthening on Labour Based Technology at ATT1	T	Mbeya	2005.10-2011.2
Upgrading Masasi-Mangaka Road (Phase I, II, III)	G	Masasi	2007.11-2011.9
Project for widening of New Bagamoyo Road	G	Dar es Salaam	2010.2-2014.12
Arusha-Namanga-Athi River Road Development	L	Arusha	2007.3-2011.6
Road Sector Support Project	L	Dodoma, Iringa, Ruvuma	2010.5-2013.12
Capacity Building for the Customs and Administrations of the Eastern African Region Phase2	T	Tanzania, Kenya, Uganda	2009.9-2013.9
Advisor of Regional Infrastructure Development for East African Community Secretariat	T	Arusha	2010.9-2012.3
(3) Infrastructure (Energy)			
Capacity Development of Efficient Distribution and Transmission Systems	T	Dar es Salaam	2009.8-2014.8
Reinforcement of Transmission and Distribution Facilities in Oysterbay Substation	G	Dar es Salaam	2008.5-2011.3
Iringa-Shiranya Backbone Transmission Investment Project	L	Iringa, Dodoma, Singida, Shiranya	2010.12-2014.11
(4) Infrastructure (Water)			
Study on Rural Water Supply in Tabora Region	T	Tabora	2009.9-2011.5
Rural Water Supply in Mwanza and Mara Regions	G	Mwanza, Mara	2009.5-2012.2
(5) Governance			
Strengthening Participatory Planning and Community Development Cycle for Good Local Governance	T	Dodoma, Coast, Morogoro	2009.10-2013.5
Local Governance Advisor	T	Dodoma	2010.9-2012.9
LGDG Basket Fund	G	Whole Country	2008.7-2011.6
LGRP2 Basket Fund	G	Whole Country	2009.7-2011.6
Capacity Development for Internal Audit	T	Dar es Salaam	2009.9-2012.9
(6) Health			
Capacity Development for Regional Referral Health Management	T	Whole Country	2008.4-2011.3
Project for Strengthening Development of Human Resources for Health	T	Dar es Salaam	2010.11- 2014.11
Health Systems Strengthening for HIV and AIDS Services Project	T	Dar es Salaam	2010.10-2014.10
Test kits and STD drugs for HIV/AIDS Control	G	Whole Country	2009.2-2012.3
(7) Education			
In-Country Training for Educational Management	T	Whole Country	2009.10-2012.6
Training for Secondary School Science and Mathematics Teachers	T	Whole Country	2009.7-2012.6
(8) Private Sector			
Industrial Development Advisor for Ministry of Industry, Trade and Marketing	T	Dar es Salaam	2008.1- 2012.1
(9) Regional Development			
African Institute for Capacity Development Phase3	T	Tanzania, Kenya, Uganda	2007.9-2012.6
(10) Tourism			
Project for the Improvement of Display and Audiovisual Equipment for Visitor Centre on Ngorongoro Conservation Area	G	Arusha	2010.10-2013.2
(11) Technical Training Programme			
Technical Training Programme	T	Whole Country	
(12) Volunteer Programme			
Japanese Overseas Cooperation Volunteers	T	Whole Country	
(13) General Budget Support			
General Budget Support / PRSC	L	Whole Country	2003.7-2010.6